



World Health
Organization

WHO GLOBAL TASK FORCE ON CHOLERA CONTROL

Maradhi makali ya kuhara katika mazingira magumu ya dharura:

HATUA MAHUSUSI

Uamuzi wa hatua za
maandalizi na mwitikio

KUSUDI

Ukurasa huu umetungwa kusaidia:

- Kutambua hatua muhimu za kuzuia magonjwa ya kuhara wakati mgumu wa dharura
- Kutayarisha na kuongoza mwitikio wa mlipuko

TATIZO

Hali ngumu ya dharura ni hali ambayo inaadhiri idadi kubwa ya watu ambao wanakabiliwa na vita au vurugu zingine, njaa, watu kuhamahama maeneo yao kutokana na vifo na uchafu kuongezeka.

Katika maeneo sugu ya maradhi, kila aina ya maafa (maafa ya asilia au maafa yasababishwayo na binadamu) ambayo inaathiri upatikanaji wa maji safi na usafi/udhibiti afya (sanitation), inaweza kusababisha milipuko ya magonjwa ya kuhara. Magonjwa haya husambazwa kwa njia ya maji machafu yenye kinyesi, au chakula/vinywaji visicho salama. Kuna aina mbili za milipuko:

- Ugonjwa wa ghafla wa kuharisha maji maji na kwa kasi sana: **kipindupindu**
- Muharo mkali wa kuharisha damu: **Shigella dysentery**

MUHIMU NI

KWA UJUMLA

- Fuatilia maendeleo ya hali kwa makini ili mipango na vitendo viambatane au vikubaliane wakati wote.
- Tumia data ambazo zinakuongoza kuhusiana na kinga, hatua za maandalizi, na mwitiko.
- Onyo likitolewa mapema na hatua za maandalizi kwa milipuko zikichukuliwa, kuenea kwa kipindupindu na shigella inaweza kuzuilika.
- Wakati wa hali ngumu ya dharura, ni muhimu kuwa na ratiba nzuri kati ya viongozi na wahusika wa ngazi mbali mbali.
- Mfumo mzuri wa mawasiliano ni chombo muhimu kwa uangalizi.

USIMAMIZI WA UGONJWA

- Usimamizi mzuri unaweza kuokoa maisha.
- Maji ya chumvi (ORS) lazima ipatikane kwa urahisi katika zahanati za vijijini.
- Utumiaji mapema wa Maji ya chumvi (ORS) ni muhimu.

KUZUIA

- Tafuta na komesha chanzo cha maambukizi haraka iwezekanavyo.
- Imarisha utumiaji wa maji safi wakati wa milipuko.
- Ili kudumisha afya na kupunguza hatari za matokeo ya milipuko ya magonjwa ya kuhara kwenye kambi za wakimbizi, ugawaji wa maji safi na salama iwe hatua ya kwanza kabisa.
- Usafi wa mazingira huzuia kusambaa kwa maradhi ya kuhara.
- Tabia binafsi za usafi zitabadilika tu, ikiwa jamii nzima itashirikishwa.
- Kipike, kimenye, au kiache.
- Kuuu viini vya maradhi na kufuata utaratibu maalum wa usafi ni muhimu kwenye mazishi.

1. Hatua mahususi zinazohusiana na vigezo vinavyoweza kusababisha maradhi ya kuharisha

1.1 Ukosefu wa maji

- Kwa kutumia elimu ya afya, himiza utumiaji wa maji safi na salama ya kunywa wakati wa milipuko.
- Kwenye kambi za wakimbizi, ugawaji wa maji safi na salama iwe hatua ya kwanza ili kuendeleza afya ya watu na kupunguza hatari ya milipuko ya maradhi ya kuhara
- Tafuta na komesha chanzo cha maambukizo haraka iwezekanavyo.

KUTATHMINI	CHANZO CHA TAARIFA	YANAYOHITAJIKA ANGALAU	HATUA YA MAANDALIZI	MWITIKIO
<p>Kiasi na ubora wa maji</p> <p>Chanzo cha maji:</p> <ul style="list-style-type: none"> - maji ya bomba - maji ya kisima - mengineyo 	<p>Watu wahusika, mashirika ya misaada yanayohusika</p> <p>Mamlaka ya maji, mashirika ya misaada, utembeleaji wa maeneo</p>	<p>Si chini ya lita ishirini za maji safi na salama ya kunywa kwa mtu mmoja kwa siku</p> <p>Kisima chenye maji salama, ambapo maji chafu hayawezi kuingia (protected well)</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Kwa kushirikiana na mamlaka ya maji, ongeza upatikanaji wa maji safi na salama kwa urahisi, angalau kwenye maeneo mahususi. • Ugavi wa maji mijini: <ul style="list-style-type: none"> - weka njia mpya za kupata maji safi na vyoo na vifaa vya kuondosha maji machafu na takataka (sanitation facilities) - kagua na boresha ubora wa maji safi ya kunywa • Vijijini: <ul style="list-style-type: none"> - ongeza idadi ya visima vyenye maji salama, ambapo maji machafu hayawezi kuingia (protected wells) - anzisha usafishaji wa maji visimani kwa kutumia chlorine 	<ul style="list-style-type: none"> • Wakati wa mlipuko kwenye kambi za wakimbizi (eneo maalum) hakikisha: <ul style="list-style-type: none"> - angalau lita ishirini za maji kwa kila mtu kwa siku - uhifadhi bora wa maji nyumbani (kwenye vyombo vya kiplastiki na mdomo mdogo) • Kwenye hatua za kwanza na wakati hali ikiwa ni ngumu sana, tia chlorine kwenye vyanzo vya maji, na weka chlorine moja kwa moja ndani ya vyombo vya kuhifadhi maji • Wakati wa mlipuko kwenye maeneo wazi (kwa mfano mjini, vijijini): <ul style="list-style-type: none"> - imarisha udhibiti wa kusafisha maji kwa kutumia chlorine kuanzia yanakotoka hadi kumfikia mtumiaji - hakikisha usafishaji wa maji kwa kutumia chlorine nyumbani kwa watu (au angalau utumiaji wa maji yaliyochemshwa) - zidisha ukaguzi kuhusiana na uhifadhi bora wa maji safi
<p>Uchafu wa maji</p> <p>Kwenye chanzo cha maji:</p> <ul style="list-style-type: none"> - kwa njia ya vinyesi vya watu wanaoaka sehemu hii - kwa mafuriko - mengineyo <p>Wakati wa kusafirisha Uwekaji wa maji nyumbani</p> <p>Uongezekaji ghafala wa idadi ya watu</p>	<p>Utembeleaji wa maeneo, mashirika yanayotoa misaada, utembeleaji wa makaya</p>	<p>Vyoo vijengwe zaidi ya mita 30 kutoka chanzo cha maji; Watu wasijisaidie karibu na vyanzo vya maji, vyombo vya kuhifadhi maji viwe vya kiplastiki (visiwe vya metali)</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Elemisha watu kuhusu matumizi ya chlorine nyumbani kwao. • Gawa maji yaliyosafishwa na chlorine wakati wa milipuko. • Wafahamishe watu kuhusu umuhimu wa kusafisha vyombo vya kuhifadhi maji. 	
	<p>Viongozi wa mitaa, mashirika yanayotoa misaada</p>		<ul style="list-style-type: none"> • Tafuta (vyanzo vya) maji zaidi ili kuweza kukabiliana na uongezaji wa watu 	<ul style="list-style-type: none"> • Maji yanaweza kusambazwa na magari/tenki hadi hapo visima vipya vitakapochimbwa

1.2 Mazingira machafu

- Mazingira safi huzuia kusambaa kwa maradhi ya kuhara.

KUTATHMINI	CHANZO CHA TAARIFA	YANAYOHITAJIKA ANGALAU	HATUA YA MAANDALIZI	MWITIKIO
<p>Vyoo havitumiwi (kwa sababu za kimila)</p>	<p>Wenyeji wa mahali Mamlaka ya serikali za mitaa</p>		<ul style="list-style-type: none"> • Ongeza idadi ya nyenzo za kimila za utupaji wa vinyesi vya watu. • Jaribu kutafuta aina ya choo 	<ul style="list-style-type: none"> • Mwanzo wa hali ngumu ya dharura, Inawezekana kutenga maeneo maalum yatakayotumika kwa kujisaidia,

Ukosefu wa vyoo:	mitaa			
– hakuna maeneo	Utembeleaji wa mahali, mahojiano na watu wanaoaka mahali, mashirikira ya misaada	Kwenye kambi za wakimbizi na wakati wa umati wa watu, angalau choo kimoja kwa watu ishirini	• Jaribu kutaruta aina ya choo kinachokubalika kimila, na kinachofaa kwa aina ya udogo uliopo sehemu hii na ambacho ni cha bei nafuu.	yatakayotumika kwa kujisaidia, lakini lazima yvoo vichimbwe haraka iwezekanavyo.
– aina ya udongo				
– gharama				

1.3 Tabia za usafi wa mtu binafsi zisizoridhisha

■ Tabia zanzozhusiana na usafi wa mtu binafsi zinabadilika tu, kama jamii nzima itashirikishwa.

KUTATHMINI	CHANZO CHA TAARIFA	YANAYOHITAJIKA ANGALAU	HATUA YA MAANDALIZI	MWITIKIO
Ukosefu wa maji	Utembeleaji wa maeneo; kagua sehemu zote ambapo maji yanaweza kupatikana	Lita ishirini za maji kila mtu kwa siku (ya kunywa na matumizi mengine ya kiasya)	<ul style="list-style-type: none"> • Endelea kueleleisha wananchi kuhusu kipindupindu na maradhi mengine ya kuhara na njia za kuyazuia: <ul style="list-style-type: none"> – endelea tabia binafsi ya kiasya – Tilia mkazo wa utumiaji wa sabuni au majivu kwa kunawa mikono, hasa baada ya haja kubwa – tunga kanuni ndogondogo kuhusu kipindupindu na uzuiaji wa maradhi mengine ya kuhara, pia namna ya kuhudumia mgonjwa nyumbani • Elimisha wafanyakazi wa sekta ya afya na wafanyakazi wengine wa serikali wanaohusika na utangazaji wa habari rasmi kuhusu kutoa na kusambaza elimu ya kuzuia kipindupindu. 	<ul style="list-style-type: none"> • Wakati wa mlipuko, himiza utumiaji wa vyoo na vyombo vingine vya kuondosha maji machafu na takataka. • Tumia njia zote za mawasiliano (redio, televisheni, magazeti) ili kutangaza habari kuhusu mlipuko na kanuni za usafi zinazotakiwa kufuatwa. • Tumia aina zote za idhaa (utawala wa mji au kijiji na viongozi wa dini, shule, wafanyakazi wa afya wa jumua, na viongozi wa vijiji) kusambaza taarifa kuhusu kanuni za usafi wa mwili. • Gawa sabuni sehemu ambako hazipatikani.
Usafi wa mwili usioridhisha	mahojiano na wenyeji	Kunawa mikono kwa sabuni kabla ya kutayarisha chakula na kula chakula		
Upungufu wa ujuzi wa hatari iliyopo wakati wa kuhudumia wagonjwa wa kipindupindu na maradhi mengine ya kuhara	Mahojiano na wenyeji na wafanyakazi wa serikali wanaohusika na utangazaji wa taarifa	Mtenge mgonjwa nyumbani Nawa mikono kwa sabuni kila baada ya kuhudumia wagonjwa au kushika vitu vyao		

1.4 Usafi wa vyakula usiotosheleza

■ Kipike, kimenye, au kiache.

KUTATHMINI	CHANZO CHA TAARIFA	YANAYOHITAJIKA ANGALAU	HATUA YA MAANDALIZI	MWITIKIO
Nyumbani:	Mamlaka ya serikali za mitaa, mahojiano, mashirikira ya misaada	Wakati wa mlipuko, kula chakula kilichopikwa kwa muda huo huo. Kama chakula kimevekwa kwa muda mfupi, kipashe moto (mpaka kichekeme tena) kabla ya kula. Kula matunda yanayomenyeka	<ul style="list-style-type: none"> • Imarisha elimu ya afya kuhusu: <ul style="list-style-type: none"> – Kula chakula kilichopikwa tu wakati wa mlipuko – safisha mbogamboga kwa maji safi na salama (maji yaliyochemshwa au kutiliwa dawa) – kula matunda ambayo yanamenyeka tu • Hakikisha kwamba kuna ukaguzi bora na wa kutosha kwenye migahawa/mamalishe na sehemu nyingine panapouzwa vyakula. 	<ul style="list-style-type: none"> • Mafunzo ya kiasya lazima yasisitize umuhimu wa taarifa na mafundisho maalum kuhusu utayarishaji, uwekaji na ulaji wa chakula. • Mradi wa chakula bora na chenye usalama uimarishwe. • Wafanyakazi wa afya na usafi wa mazingira lazima wawe makini kukagua jinsi vyakula vinavyotuzwa.
Mfuatano wote wa chakula	Utembeleaji wa maeneo, mamlaka ya usafi na usalama wa vyakula			
Ukosefu wa usafi na usalama wa vyakula kwenye masoko na migahawani/mamalishe na vyakula vinavyouzwa				

1.5 Kuzika watu waliokufa kwa kipindupindu

- Kwenye mazishi ni muhimu kua viini vya maradhi na kufuata utaratibu maalum wa usafi.

KUTATHMINI	CHANZO CHA TAARIFA	YANAYOHITAJIKA ANGALAU	HATUA YA MAANDALIZI	MWITIKIO
Uwekaji maiti nyumbani: <ul style="list-style-type: none"> – kwa muda gani? – kwa hali gani? 	Wenyeji mahojiano, mashirika ya misaada	Kama inawezekana mazishi lazima yafanyike masaa machache baada ya kifo maiti ihifadhiwe ndani ya mfuko wa plasitiki ili kuzuia mambukizo na usambazaji wa vimelea vya bakteria viitwavyo Vibrio cholera	<ul style="list-style-type: none"> • Arifu watu kuhusu hatari kubwa ya kuambukizwa wakati wakihudumia maiti na wakiuweka nyumbani. • Eleza tahadhari za lazima: <ul style="list-style-type: none"> – safisha maiti kwa kutumia chlorine 2% (mzimuo wa asilimia mbili) – jaza mdomo na mkundu wa maiti kwa pamba iliyorowekwa katika mzimuo wa chlorine – nawa mikono baada ya kuhudumia maiti au kushika – safisha nguo za marehemu na nguo zake za kitandani kwa kuchemsha kwa dakika tano. • Jaribu kufupisha utaratibu wa mazishi. • Imarisha aina zote za kanuni za kiafya wakati wa matayarisho ya mazishi na utaratibu wake. • Chagua na elimisha kikosi maalum cha mazishi, ili kuhakikisha kwamba utaratibu wa mazishi unatekelezwa inavyopaswa. 	<ul style="list-style-type: none"> • Hakikisha tahadhari zote zimeeleweka na kufuatwa kwa makini. • Kama inawezekana mfanyakazi wa afya wa kijiji, aliyepata mafunzo kabla, akagwa kama kanuni zote za uziujaji zimefuatwa vizuri na kutumiwa wakati wa mazishi na shughuli zingine zinazohusika.
Utaratibu wa mazishi: <ul style="list-style-type: none"> – mahudhurio? – kanuni maalum? – maakuli ya kilioni? 	Wenyeji mahojiano	Ufuataji wa kanuni za afya kama zilivyoelezwa wakati wa hatua za maandalizi		

2. Hatua mahususi zinazohusiana na vigezo vingine vinavyoweza kusababisha maradhi ya kuharisha

2.1 Upungufu wa huduma za afya

KUTATHMINI	CHANZO CHA TAARIFA	YANAYOHITAJIKA ANGALAU	HATUA YA MAANDALIZI	MWITIKIO
Maradhi ya kuambukiza na mfumo wa uangalizi: <ul style="list-style-type: none"> – ukusanyaji wa data – uthibitisho wa maabara – uchanganuzi wa data – mwitikio/majibu ya walengwa (feedback) – mfumo wa kutoa tahadhari/onyo mapema 	Idara ya Afya na jamii kwenye ngazi mbalimbali (taifa, mkoa, wilaya), mashirika ya misaada	Idadi ya wagonjwa na vifo kwa wiki kufuatana na uthibitisho wa maabara	<ul style="list-style-type: none"> • Imarisha mfumo wa uangalizi: <ul style="list-style-type: none"> – tumia njia zinazooleweka na sanifu kufafanua hali ya mgonjwa – kuza na sanifisha taratibu za kukusanya na kuchanganua data, kwa ngazi zote (kimahali, siku za mlipuko) – hakikisha kwamba ripoti za wiki zitolewe na data zote zichanganuliwe mara kwa mara – anzisha kusanifisha “aina ya uvumi” kwa watu ambao si wafanyakazi wa afya – elimisha wafanyakazi wa afya wa serikalini na wafanyakazi wa afya vijijini 	<ul style="list-style-type: none"> • Anzisha mfumo wa kutoa tahadhari mapema: <ul style="list-style-type: none"> – sambaza fomu “aina ya uvumi” (fomu ya tahadhari, fomu ya onyo) – anzisha utambuaji wa wagonjwa wakati wa kutembelea nyumbani kwao kwenye kambi za wakimbizi – kama inawezekana anza kutoa taarifa kila siku – tuma kikosi cha ukaguzi ili kuthibitisha mlipuko na kutambua chanzo cha maambukizi (maji, chakula) • Funqua vituo maalum vya matibabu wa
Nyenzo za Huduma za afya Vituo vya afya	Wizara ya Afya Kutembelea vituo vya afya	Kuweka vituo vya ORS Kuweka vituo		

Vituo vichache vya afya Idadi ya vituo/didadi ya watu	Kutumbelea vituo vya afya vinavyohusiana na afya, taarifa ya ziara, taarifa	Kuweka vituo vya matibabu vya kipindupindu
Umbali Msongamano wa wagonjwa kwenye vituo vya afya nyenzo	kutoka mlipuko iliyopita.	Upatikanaji wa miongozo ya matibabu
Ukosefu wa wafanyakazi wenye ujuzi	Wizara ya Afya	Wafanyakazi watatu wa afya waliopata mafunzo maalum, kwa kila kituo cha matibabu ya kipindupindu, mfanyakazi mmoja wa afya aliyepata mafunzo maalum, kwa kila kituo cha ORS
Ukosefu wa madawa	Mahojiano na wafanyakazi, vitabu vya kuorodhesha madawa, vifaa na vile vilivyotolewa kwa msaada	Vifaa vya wakati wa dharura viweze kupatikana: Interagency diarrhoeal disease kits
Uratibu duni wa shughuli	Mahojiano na washirika wakuu na mashirika yasiyo ya serikali (NGO)	Mikutano mara kwa mara wakati wa mlipuko

- serikalini na wafanyakazi wa afya vijijini kuhusu mfumo wa uangalizi na mfumo wa kutoa tahadhari/onyo mapema
- tambulisha maabara yanayotoa uthibitisho
- Usimamizi wa ugonjwa:**
 - tambulisha mahali maalum ambapo panafaa kuweka vituo vya matibabu ya kipindupindu na vituo vya ORS. Ikiwa lazima angalia na endeleza upatikanaji wa maji na hali ya vyoo
 - tambua wafanyakazi wa afya wanaohusika na vituo vya matibabu ya kipindupindu au vituo vya ORS na uwafunze kuhusu usimamizi wa ugonjwa, kanuni za usafi na njia muhimu za kuzuia maambukizi (pamoja na namna ya kusafisha maiti na kemikali ya kuzuia maambukizi)
- Gawa vifaa vya dharura (ORS, Ringer Lactate, chlorine, kifaa cha kusafirishia sampuli, kemikali za maabara (reagents)).
- Mfumo wa uangalizi na miongozo ya usimamizi wa ugonjwa. ukubaliane na hali halisi ya mahali.
- Uratibu:**
 - unda kikosi maalumu kinachohusika na magonjwa sugu, husisha vikundi vyote maalum (idara za afya, maji, makaro, maelezo, na elimu), wanasiasa watoaji uamuzi, mashirika yasiyo ya serikali, Mashirika ya Umoja wa Mataifa
 - kubaliana kuhusu kusanifisha mfumo wa uangalizi na usimamizi wa ugonjwa kuhudumia mgonjwa kuhakikisha ufuatiliaji
 - toa changamoto kuhusu uratibu wa kuhusisha sekta mbalimbali kuhusu kuzuia na kudhibiti ugonjwa, uunganishaji wa utaratibu uliopo
 - Pangia kazi na majukumu
- hakikisha kuna ugavi wa kudumu wa maji safi na salama kwenye vituo vya matibabu ya kipindupindu na vituo vya ORS
- hakikisha kuna upatikanaji wa madawa na ugavi wa vifaa vipya kukiwa na upungufu.
- wakumbushe kuhusu usimamizi bora wa ugonjwa
- tilia mkazo kuhusiana na usafi na kuaa viini vinavyosababisha maradhi kwa kutumia harakati zote kiafya (fikia hadi mashirika yanayo husika na uchanjaji, na ushauri, n.k)
- gawa miongozo ya kitaifa kama inapatikana, au miongozo ya shirika la afya la ulimwengu.
- Hakikisha ugawaji wa vifaa wakati wa mlipuko na ongeza vifaa vipya vikipingua.
- Hakikisha uratibu mzuri kati ya wahusika mbalimbali.
- Itisha mikutano kila mara ili kubadilishana au kufahamishana taarifa kuhusu uorodheshaji wa vifaa vya maradhi ambukizi, kupanga namna ya kuyakabili.

2.2 Vituo vya afya visivyofikika

KUTATHMINI	CHANZO CHA TAARIFA	YANAYOHITAJIKA ANGALAU	HATUA YA MAANDALIZI	MWITIKIO
Maafa ya asilia	Idadi ya wenyeji	Akiba ya vifaa vya dharura kwenye maeneo yaliyo hatarini	Katika maeneo yaliyotengwa kwa vita, mafuriko, n.k. ni muhimu: <ul style="list-style-type: none"> fundisha wafanyakazi wa afya wa vijijini na wafanyakazi wa wizara ya afya gawa vifaa vya dharura weka mfumo mzuri wa mawasiliano kuhusu uangalizi 	<ul style="list-style-type: none"> Anzisha mfumo wa mawasiliano kutoa msaada na mwitikio wa walengwa. Fuatilia mlipuko unavyoenda kwa kutumia mfumo huu wa mawasiliano.
Si ya salama				

MPANGO WA HARAKATI - HATUA MAHUSUSI

KUTATHMINI

Kutathmini hali halisi ilivyo ni ya msingi kwa kila mpango wa harakati. Malengo yake ni:

- kutathmini uzito wa dharura, tishio la maradhi ya kuambukizana kwa jamii, na idadi ya watu ambao wako hatarini¹
- kufafanua hali ya mlipuko na kuamua hatua gani zichukuliwe

Kutathmini pia in muhimu kwa matayarisho ya kupata mwitiko wa kuridhisha. Taarifa zifuatazo zinahitajika na labda zinapatikana kutoka kwa viongozi wa serikali, mashirika ya misaada, na Mashirika ya Umoja wa Mataifa:

- maelezo kuhusu maafa (mgogoro kati ya wenyeji, vita, majanga ya mazingira) na labda mabadiliko yake baadaye
- maelezo ya kijiografia kuhusu maeneo yaliyoathirika (hali ya hewa, kama ipo kwenye upeo wa milima au siyo, kama maji yanapatikana)
- fursa ya kuingia kwenye eneo (hali ya barabara, hasa wakati wa masika, eneo la bandari, au kiwanja cha ndege, hali duni ya usalama)
- kiasi cha watu (idadi ya wenyeji, idadi ya wahamiaji/wakimbizi, mgawanyo kwa umri na jinsia, idadi ya watu wapya watakaofika na tarehe ya kufika (kwa wastani))

HATUA YA MAANDALIZI

Awamu ya maandalizi ni kipindi cha kuendeleza na kutekeleza hatua zote zinazohusiana na kinga na ufafanuzi wa mahitaji ili kupambana na mlipuko wa aina yoyote. Shughuli za hatua za maandalizi zitegemea kufuatana na matokeo ya kutathmini.

MWITIKIO

Mwitikio wa mlipuko ni utekezaji wa shughuli zote zilivyopangwa. Kama mlipuko wa maradhi unatokea ghafula sana, labda hapatakuwa na muda wa awami ya hatua za maandalizi. Hata hivyo:

- Kutathmini hali halisi ni muhimu; data za mwanzo lazima zikusanywe haraka sana na zichanganuliwe kabla ya kumaliza kutathmini
- Mwitikio lazima uanzwe haraka; huenda mwitikio itabidi ubadilishwe kutokana na hali halisi inavyoendelea na pale ambapo ukusanyaji na uchanganuzi wa data ukishakamilika

¹ Idadi ya watu waliyomo hatarini kuambukizwa na maradhi ya kuhara, ikiwemo kipindupindu, kutokana na:

- Idadi ya watu walioambukizwa (=Attack rate (AR)) ya miaka iliyopita, kama inajulikana
- Idadi ya watu walioambukizwa (AR) ya 0.2% katika maeneo yenye maradhi
- Idadi ya watu walioambukizwa (AR) ya 0.6% katika maeneo yenye maradhi yenye hali mbaya ya usafi/udhibiti afya, kwenye $AR = (\text{jumla ya watu walioambukizwa}) / (\text{idadi ya watu}) \times 100$. Wakati wa hali ya dharura, idadi ya watu ambao wako hatarini lazima ikadiriwe kila mara.

*The Swahili version of this document has been supported by
the BILL & MELINDA GATES FOUNDATION.*

**Global Task Force on Cholera Control
World Health Organization
20 Avenue Appia • 1211 Geneva 27 • Switzerland
E-mail: cholera@who.int**

For more information, see the cholera web site: www.who.int/cholera



© World Health Organization 2011

All rights reserved. Publications of the World Health Organization can be obtained from WHO Press, World Health Organization, 20 Avenue Appia, 1211 Geneva 27, Switzerland (tel.: +41 22 791 3264; fax: +41 22 791 4857; e-mail: bookorders@who.int). Requests for permission to reproduce or translate WHO publications – whether for sale or for noncommercial distribution – should be addressed to WHO Press, at the above address (fax: +41 22 791 4806; e-mail: permissions@who.int).

The mention of specific companies or of certain manufacturers' products does not imply that they are endorsed or recommended by the World Health Organization in preference to others of a similar nature that are not mentioned. Errors and omissions excepted, the names of proprietary products are distinguished by initial capital letters.

All reasonable precautions have been taken by the World Health Organization to verify the information contained in this publication. However, the published material is being distributed without warranty of any kind, either expressed or implied. The responsibility for the interpretation and use of the material lies with the reader. In no event shall the World Health Organization be liable for damages arising from its use.

WHO/CDS/CPE/ZFK/2004.6 Rev. 1